

## Maswali

1. Nani aliondoka Israeli?
2. Mbona walitoka?
3. Walienda wapi?
4. Nini ilifanyika kwa Elimeleki?
5. Maloni na Kiloni walioa nani?
6. Nini ilifanyika kwa Maloni na Kiloni?
7. Nani alirudi Israeli na Naomi?
8. Ruthu aliokota nafaka kwa shamba la nani?
9. Boazi alioa nani?
10. Nani alikuwa mijukuu wa Boazi na Ruthu?

## Majibu

1. Elimeleki, Naomi na wanao wavulana waliondaka Israeli.
2. Waliondoka kwa ajili ya njaa.
3. Walienda Moabu.
4. Elimeleki alikufa.
5. Maloni na Kiloni walioa Ruthu na Orpa.
6. Maloni na Kiloni walikufa.
7. Ruthu alirudi Israeli na Naomi.
8. Ruthu aliokota nafaka kwa shamba la Boazi.
9. Boazi alimuoa Ruthu.
10. Daudi alikuwa mijukuu wa Boazi na Ruthu.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM



**Awamu ya 1 Mwaka wa 1**

## 22 Ruthu na Naomi

### Marejeo

Ruthu

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba tukiamini, kusudi ya Mungu hufanyika hata mambo yasipoenda vizuri

### Maneno maalum

1. Njaa + Elimeleki + Naomi + Moabu + Maloni + Kiloni + wake + Ruthu + Orpa + kifo.
2. Enda nyumbani + hatukuachi + Mungu wako
3. Rudi + Bethlehemu + tupu (bila kitu)
4. Shamba + okota nafaka + Boazi
5. Lala miguuni + ahadi + jamaa + mke
6. Obedi + Yese + Daudi

**22.1** Kulikuwa na wakati moja, njaa ikawa nyingi katika nchi ya Israeli. Mtu aitwae Elimeleki, mkewe na wanawe Maloni na Kiloni wakatoka Bethlehemu na kuenda kwa nchi ya Moabu. Waliishi huko siku nyingi na Elimeleki akafa. Maloni na Kiloni walioa wanawake wa Moabu. Wake zao waliitwa Ruthu na Orpa. Bunde tu Maloni na Kiloni walikufa. Naomi aliachwa pekee na wakweze (wake zake).

**22.2** Baadaye, Naomi alisikia kwamba kulikuwa na chakula Israeli. Aliamua kurudi nyumbani. Naomi aliwaambia wakweze Ruthu na Orpa, "Rudi nyumbani kwa sababu mimi ninarudi kwa nchi ya Israeli."

Naomi aliwabusu hali wamehuzunika. Orpa alirudi lakini Ruthu hakumuacha Naomi. Alisema, "Nitaenda na wewe, Mungu wako atakuwa Mungu wangu na watu wako watakuwa watu wangu."

**22.3** Kwa hivyo Naomi na Ruthu walirudi Bethlehemu. Walipofika , watu wote walifurahi kuwaona. Wakauliza , "Je! Huyu ni Naomi ?" Aliwaambia, "Mungu amenitesa sana; Amenirudisha nyumbani nikiwa tupu." Hakukumbuka kwamba amerudi na Ruthu. Ruthu alimpenda na kumsaidia kwa vyo-vyote.

**22.4** Kulikuwa wakati wa kuvuna shayiri (kama ngano). Lakini Naomi na Ruthu walikuwa maskini, hawakuwa na shamba la shayiri. Ruthu alienda kuokota nafaka nyuma ya waliokuwa wakivuna wakiangusha. Naomi alikuwa na jamaa yake alieitwa Boazi na kukatukia Ruthu alienda kwa shamba moja la Boazi.



Boazi alipokuja shambani alisema na watumishi wake akawauliza, "Ni nani huyu mwanamke kijana?" Walimwambia ni mwanamke kijana Mmoabu aliyejeka na Naomi.

Boazi alizungumza na Ruthu na akamwambia, amesikia mema yote aliyomtendea Naomi. Akamuuliza abaki shambani mwake ili kila siku ajaze kikapu.

Ruthu aliokota nafaka kwa siku nzima na kumpelekea Naomi.wakati wote aliokota kwa shamba la Boazi. Boazi aliwaambia watumishi wawe wakile chakula naye na kumuongezea nafaka kwa kikapu chake.

**22.5** Naomi kwa mawazo yake aliona Boazi anaweza kumchukuwa Ruthu nyumbani kwake. Alituma Ruthu aende usiku walipokuwa wakipura shayiri. Boazi alipokuwa amelala bila kujua, Ruthu alijilaza miguuni pake. Usiku wa manane Boazi aliamka na kumuona Ruthu. "Mbona uko hapa?"aliuliza. Ruthu alijibu, "Wewe ni jamaa wa Naomi, tafadhali unijali."

Boazi alimpa Ruthu nafaka nyingi na kumwambia aende nyumbani. Siku iliyofuata alimwelezea jamaa wa karibu zaidi na Naomi lakini hangeweza kulinda jamii yake pamoja na Ruthu. Naye alifurahi kujua kwamba Boazi alikuwa tayari kumchukuwa. Boazi alifanya mpango wa kumchukuwa Ruthu awe mke wake kwa maana alimpenda. Naomi alifurahi kwa sababu alimpenda Ruthu na alitaka akae vizuri.

**22.6** Baada ya Boazi kuo Ruthu, walipata mtoto aitwae Obedi. Naye alipokua akapata mtoto aitwae Yeso. Yeso alikuwa baba wa Daudi aliyekuwa mfalme wa Israeli.